

CHUO KIKUU CHA MTAKATIFU AGUSTINO CHA TANZANIA
OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO TAALUMA
S.L.P 307
MWANZA, TANZANIA

Simu: 028 29 81186
028 29 81187
Nukushi: 028 29 81185



Barua pepe: dvcaa@saut.ac.tz
Tovuti: www.saut.ac.tz

MAHAFALI YA ISHIRINI NA SITA


Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (SAUT), Mhashamu Baba Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga wa Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, anayo furaha kutangaza kuwa Mahafali ya Ishirini na Sita (26) yatafanyika katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania kwenye Uwanja wa Raila Odinga siku ya Jumamosi tarehe 16/12/2023 kuanzia saa 2:00 asubuhi.

Mahafali yatatanguliwa na Kongamano la Wahitimu (Alumni Convocation) litakalofanyika tarehe 15/12/2023 kuanzia saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa M-15. Msemaji Mkuu atakuwa **Mh. Patrobas Paschal Katambi - Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu).**

Wahitimu wote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kulipa Tsh. 52,000/= (elfu hamsini na mbili tu) kupitia akaunti ya chuo namba 01J1053964003 - CRDB kwa ajili ya gharama ya mahafali.
2. Kuchukua majoho Jengo la Utawala kuanzia siku ya tarehe 11-15/12/2023 saa 3:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.
3. Wahitimu watapaswa kurudisha majoho baada ya mahafali kuanzia tarehe 18-20/12/2023 kabla ya saa 9:00 alasiri.
4. Kutakuwa na faini ya Tsh. 10,000/= (shilingi elfu kumi) kwa kila siku itakayozidi kwa mhitimu atakayeshindwa kurudisha joho muda uliopangwa.
5. Kufika chuoni tarehe 15/12/2023 saa 9:00 alasiri kwa ajili ya taratibu zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi kwa ajili ya mahafali.
6. Wahitimu wote wanapaswa kujitegemea wenyewe kwa gharama za usafiri, malazi na chakula kwa kipindi chote cha shughuli za mahafali.

WOTE MNAKARIBISHWA


Prof. Hossea Rwegoshora
Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma

Tel: 028 29 81186/7, Fax: 028 29 81185, Email: dvcaa@saut.ac.tz